**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MII,(OA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**
*(Barua Zote Zitumwe Kwa Mkuu* wa *Sekondari Magamba)*

Simu Na. *0767252521/0623982243*
Baruapepe:magamba
basec@gmail.com
Unapojibu Tafadhali taja:
Kumb Na. KTV/MMC/MAGSS/FI/37

Shule ya Sekondari
Magamba,
S . L. P 531,
Mpanda.

Tarehe …………………

Mzazi wa…………………………………….
S.L.P………………
Mpanda.

**Kuh; MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA.MWAKA 2021**

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii .Muhula wa kwanza wa masomo utaanza rasmi tarehe …………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe husika bila
kukosa.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**
**2.1 Sare za shule**

(a) Suruali mbili rangi ya kijani (Kwa wavulana) kitambaa aina ya esteem (Original namba 1). Klla moja *sh.15,0001=* (Elfu kumi na tano tu).

(b) Sketi mbili (2) za rangi ya kijani (kwa wasichana) kitambaa aina esteem (original namba 1) Kila moja *sl1.14,000/=* (E!fu kumi na nne tu). (Sketi ni lazima iwe ndefu kuvuka magoti ya mwanafunzi ni lazima iwe ndefu kufika kwenye kifundo (ankle) cha miguu ya mwanafunzi. Utaratibu huu umewekwa iii wanafunzi wawe na sare na mshono unaofanana.

(c) Shati mbili nyeupe za pamba zenye mikono mifupi zisizo na urembo wowote zenye mfuko mmoja juu kushoto.Kwa wasichana wa kiislam wanaovaa hijab mashati yao yawe nusu kanzu

(d) Masweta mawili rangi ya dark blue (bluu nyeusi) Kila moja sh, *13,000/=* (Elfu kumi na tatu tu)

(e) T-shirt ya shule ni damu ya m~e_yenye coller na nembo ya shule. Kila moja sh.15,0001= (Elfu kumi na tano tu). Anayeziandaa ataziweka shuleni iii zipatikane kirahisi na ziwe na nembo ya shule

(f) Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi (jozi mbili) (kwa wavulana) na (kwa wasichana) viatu nyeusi kisigino kifupi vyenye mkanda (jozi mbili)

(g) Soksi fupi nyeupe angalau jozi mbiii.
(h) Mkanda wa kuvalia suruali wa rangi nyeusi.

(i) Track suit jozi moja rangi ya bluu nyeusi, bukta, raba na fulana ya kijani isiyo na maandishi kwa ajili ya michezo.

**a) Mahitajl muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;-**

I. Ream ya karatasi moja A4 (kila mwaka) pamoja na kuwa serikali inatoa ruzuku ila uhitaji wa karatasi ni kubwa sana kwa mitihani na mazoezi ya ndani.
II. Vitabu vya masomo ya sekondari vinavyoendana na mtaala wa Elimu ya sekondari Tanzania kwa ajili kujisomea ziada mwanafunzi kama mzazi ataweza kumudu gharama zake.
III. Madaftari makubwa yasiyopungua tisa (4 quire)
IV. Mkebe wa hesabu kalamu, penseli na rula
V. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
VI. Kwanja 1, jembe Ilenye mpini, ufagio 1 wa ndani (Soft groom) na ufagio 1 wa nje wenye mpini
VII. Mkoba wa mgongoni wa kuweka madaftari

3. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni (angalia viambatanisho A, B na C.

(a) Fomu ya kupima afya ambayo inatakiwa kujazwa na daktari anayetambuliwa kisheria.
(b) Fomu ya historia ya wazazi na mwanafunzi.
(c) Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

Shule ya sekondari Magamba ipo katika halmashauri ya manispaa ya Mpanda katika mkoa wa Katavi: shule hii ipo kilometa tano (5) kutoka makao makuu ya halmashauri. Uongozi wa shule ya sekondari Magamba unakukaribisha sana.

**NB**.Si jukumu la shu Ie kushona . sare za wanafunzi, mwanafunzi husika ataelekezwa kwa mtu aliyeteuliwa na shule kwa kazi hiyo.Utaratibu huu umewekwa iii wanafunzi wawe na sare zinazofanana.

4. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAVO NA KUVATEKELEZA KIKAMILIFU.

Nakutakia maandalizi merna.

......................................

**CHRISTIAN K. SIMKOKO**
**MKUU WA SHULE**
**MAGAMBA SEKONDARI**

**KIAMBATA "A"**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**
**SHULEYASEKONDARI MAGAMBA**

Kumb.Na.KTV/MMC/MAGSS/F1/39

**HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJINGA NA SHULE HII:-**

**A. WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la Baba……………………………………………………………………………**...**Hai/Si hai
2. Jina la Mama …………………………………………………………………………**..**Hail Si hai
3. Kama Saba si hai jina la mlezi ni……………………………………………………………**..**
4. Kazil Shughuli ya Mazazil Mlezi……………………………………………………………….
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi………………………………………………………………………**..**
6. Uraia ya wazazi

- Saba Mtanzania/Si Mtanzania
- Mama Mtanzania/Si Mtanzania

SAHIHI YA BABA/MLEZI WA MWANAFUNZI

SAHIHI……………………………TAREHE……………………………….

**KIAMBATA 'B'**

MAGAMBA SECONDARY SCHOOL
FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants
Student's full name.................................................................................................................

Age Years Sex ...........................................................................................................

Blood count (red and whites)..................................................................................................

Stool examination ....................................................................................................................

Urine analysis ........................................................................................................................

Syphilis and other venereal diseases test...............................................................................

T. B test.....................................................................................................................

Eye test ...................................................................................................................................

Ears..........................................................................................................................................

Abdomen....................................................................................................................

Urine for plant test...................................................................................................................

Test for pregnancy....................................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION**

Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc

.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................

I certify that the named above is fit to pursue further studies

Station ..................................................................................Signature...................................

Date ......................................................................................Designation..............................

**KIAMBAT A 'C'**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**
*(Barua Zote Ziiumwe Kwa Mkuu wa Shute wa Sekondari Magamba)*

Kumb.Na.KTV/MMC/MAGSS/F1/38

Mkuu wa Shule,
Sekondari ya Magamba,
S . L. P 531,
MPANDA.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi…………………………………………………………….nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu -kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache. Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Sekondari ya Magamba. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazil kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Sekondari ya Magamba na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

TAREHE………………… SAHIHI YA MWANAFUNZI…………………..

MIMI MZAZI/MLEZI ………………………………………………..........................Nimeshuhudia mtoto wangu.............................................................................akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea mtoto wanqu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe…………………………………………Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………….

## FOMU Na - A
## KANUNI ZA SHULE

1. Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu,Makamu Mkuu wa shule au Mkuu wa Shule.
2. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule muda wote wa shule (Darasani) isipokuwa muda wa kazi za mikono na michezo ambapo atavaa nguo rasmi za kazi/michezo.
3. Lugha chafu. matusi, ugomvi, fltina na kupigana kwa mwanafunzi ni mwiko kabisa.
4. Mwanafunzi lazima awahi popote anapotakiwa na wakati uliowekwa.
5. Mwanafunzi ni lazima aiheshimu kazi ya darasani na nje na kuitanya viz uri. Ni lazima kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa darasani awapo shuleni.
6. Unywaji wa vileo. kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ya slgara au madawa ya kulevya ni mwiko kwa mwanafunzi Hairuhusiwi kufanya biashara yoyote shuleni.
7. Wizi wa aina yoyote ni marufuku na ni kosa kubwa kwa mwanafunzi
8. Uharibifu na upotevu wa mali binafsi au ya Umma pia ni kosa kubwa.
9. Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima. mtiifu na mwenye adabu wakati wote na kwa kila mtu. Ukaidi na ubishi kwa viongozi wake ni marufuku.
10. Wageni wa wanafunzi wanaruhusiwa kuonana na wanafunzi.baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu. wanafunzi watembelewe muda wa mapumziko.
11. Mwanafunzi haruhusiwi kuoa/kuolewa wakati akiwa bado shule. Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha marufuku kuwa na mahusiano ya mapenzi awapo shuleni au nyumbani kipindi chote cha uanafunzi wake. Akibainika atafukuzwa shule mara moja.

12 Ni mwiko kwa wanafunzi kwenda nyumba za Walimu na Wafanya kazi bila ruhusa au kibali maalum toka kwa Mwalimu mlezi/Uongozi wa shule.

13 Mapambo na nakshi za aina yoyote na mavazi ya kihuni kwa mwanafunzi ni marufuku, nywele ziwe fupi, ndevu marutuku.Mitindo ya kunyoa nywele kama pank, kunyoa kipara pasipo sababu hatutavumilia ni adhabu kali itatolewa kwa atakayefanya kinyurne na haya (Aidha kofia aina yoyote, mikanda mipana na majaketi Marufuku Kabisa shuleni). Simu haziruhusiwi ukikamatwa utapewa adhabu kali na simu yake itaharibiwa kabisa.

14 Kukataa adhabu ni kukata malezi bora ya walezi wako shule ni yenye maana ya kukataa kuwa mwanafunzi wa shule hii.

15 Mgomo wa aina yoyote ni marufuku na ni haramu katika Tanzania.Matatizo yote yatashughulikiwa kwa kufuata ngazi zilizowekwa tangu Darasani hadi Baraza la Shule. Atakaye goma au kusababisha mgomo adhabu yake ni kufukuzwa shule.

## MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

I. Wizi, Kuoa/kuolewa, Kusababisha mimba, Uasherati, Ushoga, Ubakaji, kushikwa ugoni na kupiga/kupigana.
II. Ulevi, Uvutaji wa bangi na sigara ikiwa ni parnoja na madawa ya kulevya.
III. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma Ibinatsi.
IV. Kudharau wimbo wa Taita.wimbo wa Shule na Bendera ya Taila.
V. Kugoma,kuchochea au kuongoza mgomo, ikiwa ni pamoja na kukataa adhabu kwa makusudi ikiwemo kuvuruga amani na usalama wa shule,
VI. Kushiriki au kuendekeza imani za kishirikina shuleni,
VII. Kunyanyapaa au Uonevu wa aina yoyote kwa mwanafunzi mwenzake.
VIII. Kujihusisha na siasa za chama chochote anapokuwa shuleni.
IX. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kufanya mikutano isiyo halali au kuwa na kibali.
X. kuharibu miundombinu ya shule kama viti, urnerne, maji, bomba la maji kwa makusudi
XI. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
XII. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii yote ujumla.
XIII. Kupigana mwanahrzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu atj na mtu yeyote yule.
XIV. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika . Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
XV. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
XVI. Uvutaji wa sigara
XVII. Kupata ujauzito au kutoa mimba
XVIII. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
XIX. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
XX. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
XXI. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule,
XXII. Kudharau Bendera ya Taifa
XXIII. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

............................ ........................ ..............................

**JINA LA MWANAFUNZI** **SAHIHI** **TAREHE**

............................

**MKUU WA SHULE**